

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**



**MKUTANO WA SABA**

**KIKAO CHA AROBAINI NA TISA**

**22 JUNI, 2022**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA AROBAINI NA TISA– TAREHE 22 JUNI, 2022

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

429. **MHESHIMIWA MOSHI SELEMANI KAKOSO (MPANDA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa fedha za kujenga Mabweni katika Shule ya Sekondari ya Kata ya Bulamata.

430. **MHESHIMIWA SAMWEL XADAY HHAYUMA (HANANG’):**


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali itaanza lini kutekeleza ahadi ya Makamu wa Rais ya ujenzi wa barabara za ndani kwa kilomita 10 katika Mji wa Katesh.

**431. MHESHIMIWA TECLA MOHAMEDI UNGELE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzipatia Magari ya Wagonjwa Hospitali za Wilaya za Liwale, Nachingwea na Kilwa.



**WIZARA YA NISHATI:**



**432. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, mafanikio gani yamepatikana kupitia mpango wa umeme jazilizi na lini Kituo cha kupooza umeme cha Uhuru kitafanya kazi.

**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**433. MHESHIMIWA ANTIPAS ZENO MGUNGUSI  
(MALINYI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni,  
Sanaa na Michezo:-

Je, kwa nini Makocha wa mpira wa miguu  
Tanzania hawafundishi nje ya nchi hata katika  
ukanda wa Afrika Mashariki au nchi za SADC.

**434. MHESHIMIWA MOHAMED SAID ISSA  
(KONDE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni,  
Sanaa na Michezo:-

Je, Serikali inaisaidiaje Zanzibar kupata faida  
ambazo TFF inazipata katika kuendeleza soka  
la Tanzania.

**WIZARA YA MADINI:**

**435. MHESHIMIWA NDAISABA GEORGE  
RUHORO (NGARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-


Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Wananchi wa Jimbo la Ngara wananufaika na uchimbaji wa Madini ya *Nickel*.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**436. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (MEATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha VETA katika Wilaya ya Meatu.



**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**437. MHESHIMIWA JUMA OTHMAN HIJA (TUMBATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni kwa kiasi gani lengo la Benki Kuu la kutoa mikopo kwa Sekta Binafsi limefikiwa.

## **WIZARA YA KILIMO:**

### **438. MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kujenga Bwawa la Yongoma ambalo lilifanyiwa michoro ya awali Mwaka 1984.

### **III. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali Kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Kwamba, Bunge sasa likubali Kupokea na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
22 JUNI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**